

Public education
Discover a world of opportunities

KUSOMA: KUJIFUNZIA NYUMBANI

MAWAZO ZAIDI YA KUSOMA

Kusoma pamoja

Wakati unaposoma na mtoto wako:

- Wahimize kuangalia picha katika kitabu ili kuwapa wazo kuhusiana na kuwapa wazo hadithi inaweza sumulia nini
- Zungumzia juu ya kile kinachotendeka katika hadithi na katika picha
- Waonyeshe maneno muhimu katika hadithi na uelezee maneno ambayo hawafahamu
- Wahamasishe kujiunga na maneno au misemo ya sauti mara kwa mara katika hadithi
- Acha na uulize: *Je, unafikiri ni nini kitachokea baadaye? Na ni kitu kigani kinachofanya uifikiriehivyo?* - Kubali majibu yao, hata kama sio ya haki kabisa
- Waulize kuhusu matukio na wahusika katika kitabu
- Ongea juu ya hadithi au waeleze warudie hadithi kwa maneno yao wakati wakimaliza kusoma - hii inawasaidia kutambua mwanzo, kati na mwisho wa hadithi
- Jibu maswali yao hata kama inapinga mtiririko wa hadithi - kumbuka, wemekuuliza maoni yako!

Ni muhimu sana kumpa mtoto wako sifa nyingi wanapojifunza kusoma. Wasifie wakati wanajaribu kusoma kitabu. Epuka kukosoa kama wakipinga, hata kama ina kaa rahisi kwako. Baadhi ya watoto wanahitaji mazoezi na kutiwa moyo.

Kuna vitu vingi vya kusoma ikiwa ni pamoja na mashairi ya watoto; vitabu vya hadithi; vitabu visivyo vya uongo; vitabu juu ya dinosaurs na wanyama wa nyumbani; vitabu mnavyotengeneza pamoja; hadithi za kufurahisha na mashairi; vitabu vya utani; intaneti na vitabu vya CD; vitabu vya Comic; magazeti, jarida na magazeti; vitabu vya kupika; ramani za mitaani, na kamusi.

Mbinu za kusoma

- Wakati mtoto wako anafikia neno asilolijua, watie moyo kuangalia herufi ya neno na kuwawazesha kujaribusauti ya neno yote au sehemu ya neno - wape muda wa kufanya hivyo.
- Kama unafikiria mtoto wako anafahamu neno, waulize warudie kutoka mwanzo wa sentensi na kujaribu tena. Wakati mwingine hii husaidia kuwapa wazo la neno, kwa kusikiliza hadithi yote.
- Kama haufikirii kama mtoto wako anafahamu neno, liseme kwa ajili yao na kisha kuwatia moyo kuendelea kusoma.
- Mwishoni mwa hadithi, rudia maneno ambayo mtoto wako hayafahamu na kumusaidia kuweza kutambua maana yake.

Watoto ambao hufurahia kusoma nyumbani wana uwezekano mkubwa wa mafanikio katika shughuli za kusoma shulenii mapema.



Department of
Education

**Utakuta masomo zaidi kwenye
Vifurushi vya habari za nyumbani
kwenye education.wa.edu.au.**